

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TANGAZO

- Ufugaji Mjini unaozingatia sheria na ushauri wa kitaalamu una faida na ni rafiki kwa Mazingira. Kumekuwa na tabia ya wafugaji kuachia au kuchunga Mifugo na kutiririsha au kutupa ovyo vinyesi vya mifugo hivyo kusababisha kero, ajali na uharibifu wa mazingira.
- Hivyo kabla ya kufuga na wale wafugaji ambao tayari wana Mifugo lazima wapate kibali cha kufuga mjini kutoka ofisi ya kata kupitia Afisa Mifugo wa kata, ambacho kinatolewa bure. Kibali cha ufugaji kinahusisha Mifugo yote.
- Mifugo yote ni lazima ifungiwe ndani na usafi wa mazingira uzingatiwe.
- Kwa wafugaji ambao hawatafuata sheria na kutokuwa na kibali cha ufugaji hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, kulingana na sheria zifuatazo;
 1. Sheria ndogo ya Ufugaji mjini ya mwaka 1989,
 2. Sheria ya Udhhibiti wa Mazingira ya mwaka 2004 na
 3. Public Health Act, 2009

SIKU YA KUSIKILIZA KERO ZINAZOHUSU SHUGHULI ZA MIFUGO NA UVUVI NI KILA JUMANNE SAA 3:00 ASUBUHI HADI 9:00 ALASIRI KATIKA OFISI YA MIFUGO YA MAGOMENI NA OFISI YA UVUVI MWANANYAMALA KARIBU NA HOSPITALI

**ARON T. KAGURUMJULI
MKURUGENZI WA MANISPAA YA KINONDONI**